TANGAZO LA SERIKALI NA. 74 la Tarehe 7/2/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA. 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA KAMPUNI KATIKA UJENZI, MAJARIBIO NA KUANZA KWA SKIMU YA USAMBAZAJI WA MAJI WA ENEO LA MRADI WA MAJI WA KITAIFA WA HTM NA MIJI YA KOROGWE, MUHEZA NA PANGANI KWA AWAMU YA KWANZA KWA KAMPUNI YA M/S JWIL INFRA LIMITED YA MWAKA 2025

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Kampuni katika Ujenzi, Majaribio na Kuanza kwa Skimu ya Usambazaji wa Maji wa Eneo la Mradi wa Maji wa Kitaifa wa HTM na Miji ya Korogwe, Muheza na Pangani kwa Awamu ya Kwanza kwa Kampuni ya M/S JWIL Infra Limited ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 6 Juni, 2022.

Msamaha

2. Kodi yote ya Kampuni inayotokana na Ujenzi, Majaribio na Kuanza kwa Skimu ya Usambazaji wa Maji wa Eneo la Mradi wa Maji wa Kitaifa wa HTM na Miji ya Korogwe, Muheza na Pangani kwa Awamu ya Kwanza inayopaswa kulipwa na Kampuni ya M/S JWIL Infra Limited, inasamehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafika ukomo wake baada ya Kampuni ya M/S JWIL Infra Limited kuondolewa wajibu wa kulipa Kodi ya Mapato inayotokana na utekelezwaji wa Ujenzi, Majaribio na Kuanza kwa Skimu ya Usambazaji wa Maji wa Eneo la Mradi wa Maji wa Kitaifa wa HTM na Miji ya Korogwe, Muheza na Pangani kwa Awamu ya Kwanza.

Dodoma,
30 Januari, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*